“Tuna Mioyo Iliyovunjika”: Dhuluma za kingono dhidi ya wakimbizi mjini Nairobi na Mombasa, Kenya

*Mambo Wanayopitia Wanaume, Wavulana na Wanawake Waliobadilisha Jinsia wa Asili ya Kongo, Somalia na Sudani*

# Muhtasari wa Ripoti

## Utangulizi

Hadi wakimbizi 150,000 wanaishi katika vituo vya mijini vya Nairobi na Mombasa, Kenya. Ulimwenguni kote, zaidi ya asilimia 60 ya wakimbizi sasa wanaishi mijini. Wengi, kijumuisha wale wa nchini Kenya, wanaishi katika mazingira hatari ya kudhulumiwa na kunyanyaswa. Mara nyingi wana ufikiaji usiotosha wa misaada ya kibinadamu.

Wakimbizi wengi nchini Kenya wanatoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Somalia na Sudani Kusini, ambao wamekimbia vita vya kikatili, ukiukaji wa haki za binadamu na mateso. Ueneaji wa dhuluma za kingono dhidi ya wanawake na wasichana zimesababisha mizozo katika nchi hizi, na wanawake na wasichana pia wanakabiliwa na dhuluma kubwa ya kijinsia ndani ya familia zao na jamii zao. Hakuna maelezo ya kutosha yanayojulikana kuhusu dhuluma za kingono dhidi ya wanaume na wavulana, ikijumuisha wale walio na mwelekeo tofauti wa kijinsia, utambulisho tofauti wa kijinsia na jinsi wanavyojieleza, na sifa tofauti za kingono (SOGiesC), katika mazingira haya au kama wakimbizi katika sehemu za mijini nchini Kenya.

Tume ya Wakimbizi Wanawake (WRC) ilifanya utafiti ili kubaini asili na sifa za dhuluma za kingono wa kijinsia zinazofanywa dhidi ya wanaume na wavulana wakimbizi wa kutoka Kongo, Somalia na Sudani Kusini (pamoja na wale wenye hali tofauti za SOGiesC) na wanawake waliobadilisha jinsia; dhuluma wanazofanyiwa katika nchi zao, wakati wanatoroka, na mijini Nairobi na Mombasa. Maingiliano ya dhuluma dhidi ya wanawake na wasichana pia yalichunguzwa. WRC ilifanya utafiti wa nyanjani mjini Nairobi na Mombasa mwezi Aprili na Mei 2019. Mbinu zilizotumiwa zilijumuisha mahojiano ya kutafuta maoni ya wahojiwa na wataalam 40 wa masuala ya kibinadamu na vikundi 24 maalum na wakimbizi na watu 149 wanaotafuta makazi. Chuo Kikuu cha New South Wales na Taasisi ya Utafiti wa Matibabu ya Kenya ilitoa idhini ya maadili ya kufanywa kwa utafiti huu.

## Matokeo Muhimu

1. **Dhuluma za kingono zinazohusiana na mizozo dhidi ya wanaume na wavulana zinaonekana kuwa jambo linalofanyika sana nchini DRC na Sudani Kusini. Nchini Somalia, baadhi ya wanaume na wavulana hudhulumiwa na watu wa jamii, vikosi vyenye silaha na watu wa makabila mengine; hata hivyo, ukubwa wa dhuluma hizi bado si dhahiri.** Washiriki wa utafiti waliripoti kuwa aina za dhuluma za kingono wanazofanyiwa wanaume na wavulana nchini DRC na Sudani Kusini zinajumuisha kulazimishwa kushuhudia dhuluma za kingono, ubakaji, kudhulumiwa sehemu za uzazi, na kulazimisha kuwabaka wengine. Wakimbizi walio na SOGiesC tofauti ambao walishiriki katika utafiti huu waliripoti kuwa wako katika hatari kubwa ya dhuluma, ikijumuisha dhuluma za kingono, kutoka kwa wanafamilia na wanajamii wala sio vikundi vilivyojihami lwa silaha.
2. **Mjini Nairobi na Mombasa, washiriki wote wa utafiti ambao ni wakimbizi walio na SOGiesC anuwai walikiri kuwa walifanyiwa dhuluma za kingono baada ya kuwasili Kenya, mara nyingi wakidhulumiwa mara kadhaa.** Mjini Mombasa, dhuluma za kingono dhidi ya wavulana na vijana wa kiume ambao ni wakimbizi zinaonekana kuwepo. Wanawake waliobadilisha jinsia, wanaume waliobadilisha jinsia, wavulana wenye SOGiesC anuwai, wavulana na vijana wasiombatana na watu wa familia, wakimbizi wanaouza ngono, na wafungwa huonekana kuwa katika hatari kubwa zaidi ya dhuluma za kingono, unyanyasaj na kutezwai.
3. **Dhuluma za kingono dhidi ya wanaume na wavulana hufanywa kwa njia ambazo zinaingiliana na dhuluma za kingono dhini ya wanawake na wasichana. Dhuluma za kingono dhidi ya wanaume na wavulana pia huathiri maisha ya wanajamii na wanafamilia wa kike**. Katika nchi za asili, dhuluma za kingono dhidi ya wanawake na wasichana nimekithiri. Mashariki mwa DRC na Sudani Kusini, wakimbizi walisema kwamba kulazimisha wanaume na wavulana kuwabaka na/au kushuhudia dhuluma za kingono dhidi ya wanawake na wasichana ni jambo linalofanyika sana. Wake na watoto wa waathiriwa wa kiume wanaweza kutengwa, mabinti za walionusurika wanaweza kuonekana kama wasioweza kuolewa, na kukosa uwezo wa kuwa na kipato cha kudumu kutokana na athari za kiakili na kimwili za dhuluma za kingono kunaweza kuchangia umasikini wa kifamilia na pia talaka.
4. **Madhara ya kiakili, kimwili, kijamii na kiuchumi yanayosababishwa na dhuluma za kingono ni kubwa sana.** Watoa huduma waliripoti kuwa athari za kiakili na za mwili zilizoonekana za dhuluma za kingono zilijumuisha mfadhaiko unaosababishwa na tukio la kutisha, wasiwasi, mfadhaiko na kudhihirika mwilini kwa dalili za hali ya kiakili, pamoja na jeraha la mjiko na magonjwa

ya zinaa. Manusura wanaweza kudunishwa na kudharauliwa, na matarajio ya ndoa ya wanaume makapera yanaweza kuathirika. Wavulana wanaweza kulaumiwa kwa shambulio yaliyofanywa, kutelekezwa na familia zao, au kuwa na matokeo duni shuleni.

5. **Mjini Nairobi, huduma nzuri za uhamasisho hutolewa kwa wakimbizi wa kike na wa kiume walionusurika dhuluma za kingono, pamoja na wale walionusurika wenye SOGiesC anuwai; hata hivyo, watoa huduma hawawezi kukidhi mahitaji mengi ya ulinzi na yanayohusiana na dhuluma za kingono ya wakimbizi wa mijini. Mjini Mombasa, huduma chache za dhuluma za kingono zilígunduliwa**. Kupunguzwa kwa ufadhili kwa mashirika ya huduma za kibinadamu kumetatiza utoaji wa huduma. Huduma kamili, bora za afya ya akili zinazotolewa kwa waathirika ni chache.
6. **Vizuizi vingi huzuia ufikiaji wa huduma kwa manusura wakimbizi wa mijini, ingawa viwezeshaji kadhaa vilitambuliwa vinavyowezesha ufikiaji huduma.** Vizuizi vinajumuisha ufikiaji mdogo wa rekodi za wakimbizi wa mijini, fursa chache za mapato, vikwazo vya kisheria, mitazamo hasi ya watoa huduma, ufahamu duni wa upatikanaji wa huduma, na vizuizi vya kijamii na kitamaduni. Vwezeshaji vinajumuisha sheria inayoagiza kutolewa kwa huduma isiyolipishwa ya waathiriwa dhuluma za kingono katika vituo vya afya vya serikali, kutolazimisha watoa huduma kutoa taarifa, na ufafanuzi jumuishi wa dhuluma za kingono chini ya Sheria ya Uhalifu wa Kijinsia ya Kenya (2006).

## Mapendekezo Yetu ya Juu

**Kwa Serikali ya Kenya:**

- Panua upatikanaji wa rekodi za wakimbizi kwa wakati, ikijumuisha usajili, utoaji upya wa kadi za raia wa kigeni, na michakato ya uamuzi wa hali ya wakimbizi.
- Batilisha sera zinazozuia haki ya wakimbizi ya kusafiri na kufanya kazi, na hakikisha wakimbizi wana haki ya kuishi kihalali nje ya kambi maalum.
- Ondoa sehemu ya 162 na 165 ya Sheria ya Makosa ya Jinai na kuweka ulinzi kamili kwa watu wenye SOGIESC.

**Kwa Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Wakimbizi na watendaji wengine wa ulinzi wa mijini nchini Kenya:**

- Endelea kuunga mkono Sekretarieti ya Masuala ya Wakimbizi kupanua ulinzi wa wakimbizi mijini, ikijumuisha uwekaji rekodi za wakimbizi, haswa kwa wakimbizi walio na SOGIESC anuwai.
- Endelea kupanua chaguo salama za makazi kwa wakimbizi walio katika hatari ya dhuluma za kingono na manusura walio hatarini.

**Kwa watoa huduma wa mijini nchini Kenya:**

- Anzisha au upanue ushirikiano na jamii za wakimbizi kukuza mikakati inayolenga mawasiliano ya kutoa uhamasisho kuhusu dhuluma za kingono, kukanusha imani potovu, na kufafanua jinsi, mahali na sababu za kupata huduma za watu waliodhulumiwa kingono.
- Kuunga maendeleo ya kiufundi ya watoa huduma za afya ili kuboresha matibabu ya waathiriwa wote wa dhuluma za kingono.

**Kwa wafadhili**:

- Kwa serikali wafadhili: Ongeza makazi ya wakimbizi wenye SOGiesC anuwai.
- Kwa wafadhili wote: Toa ufadhili ili kusaidia, kupanua na kuongeza miundo bora ya utoaji wa huduma za maeneo husika kwa waathiriwa wa dhuluma za kingono ambao ni wakimbizi, ikijumuisha vituo vya mijini kando na Nairobi na Mombasa.

## Tume ya Wakimbizi Wanawake

Tume ya Wakimbizi Wanawake inaboresha maisha na kulinda haki za wanawake, watoto na vijana ambao wametoroka makwao kufuatia mizozo na ghasia. Tunachunguza mahitaji yao, kutambua suluhisho, na kupendeleza mipango na sera za kuimarisha ustahimilivu wao na kuwezesha mabadiliko katika sekta ya msaada wa kibinadamu.

Ripoti kamili kwa Kiingereza, muhtasari mkuu kwa Kiswahili na muhtasari wa wachangiaji wa jamii katika Kiarabu, Kidinka, Kiswahili, Kilingala na Kisomali zinapatikana kwenye https://www.womensrefugeecommission.org/svproject.

Ili upate maelezo zaidi, wasiliana na Dale Buscher, makamu wa rais, mipango, Tume ya Wakimbizi Wanawake,
daleb@wrcommission.org
au
Dkt. Sarah Chynoweth, mkurugenzi/mshauri wa masuala ya dhuluma za kingono, Tume ya Wakimbizi Wanawake,
svproject@wrcommission.org

Oktoba 2019